

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI  
JESHI LA POLISI TANZANIA



**TANGAZO LA NAFASI ZA AJIRA**

Mkuu wa Jeshi la Polisi Tanzania ametangaza nafasi mpya za ajira ya kuijunga na Jeshi la Polisi Tanzania.

**1. Sifa za Waombaji**

- a) Awe raia wa Tanzania kwa kuzaliwa.
- b) Awe amehitimu kidato cha nne kuanzia mwaka 2019 hadi 2022 mwenye umri kuanzia miaka 18 hadi 25.
- c) Kwa waombaji wa kidato cha nne wawe na ufaulu wa daraja la kwanza mpaka la nne (Division I – IV). Kwa waombaji wenye ufaulu wa daraja la nne (Division IV) wawe na ufaulu wa alama (Point) 26 hadi 29.
- d) Wenye elimu ngazi ya Astashahada na Stashahada wawe na umri wa miaka 18 hadi 29.
- e) Awe na urefu usiopunguwa futi tano na inchi tano (5'5") kwa wanaume, na futi tano inchi mbili (5'2") kwa wanawake.
- f) Awe amehitimu mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) na Jeshi la Kujenga Uchumi (JKU) walioiko kwenye Makambi na nje ya Makambi.
- g) Awe na kitambulisho cha taifa au namba ya utambulisho kutoka mamlaka ya vitambulisho vya taifa (NIDA).
- h) Awe na afya njema kimwili na kiakili iliyothibitishwa na daktari wa Serikali.
- i) Awe hajaoa/kuolewa au kuwa na mtoto.
- j) Awe hajawahi kutumia madawa ya kulevya.
- k) Awe tayari kuhudhuria mafunzo ya awali ya taaluma ya Polisi.
- l) Awe hajaajiriwa au hajawahi kuajiriwa na taasisi nyingine ya Serikali.
- m) Awe tayari kufanya kazi za Polisi mahali popote Tanzania.
- n) Awe tayari kujigharamia katika hatua zote za usaili endapo ataitwa
- o) Asiwe na alama za kuchorwa mwilini (tattoo).
- p) Asiwe na kumbukumbu za uhalifu.
- q) Kwa waombaji wenye elimu ya kiwango cha Stashahada (NTA level 6) na Astashadaha (NTA level 5 au NVA level 3) wanatakiwa wawe na fani zifuatazo: Muziki (Music and sound production, performing arts, film and TV production), Ushonaji (Graphics and printing design, leather crafting, sewing machine maintainance, sewing operator, sign writing), Ufundi seremala (Carpentry and joinery) na Ufundu magari (Automobile mechanics, Autoelectric engineering & Autobody repairs).
- r) Waombaji watakaofaulu usaili ndio watakaochaguliwa.

## **2. Utaratibu wa kutuma Maombi**

1. Waombaji wote wanatakiwa waandike barua za maombi wao wenyewe kwa mkono (Handwriting) bila ya kusahau kuweka namba za simu, na watumie anuan: Mkuu wa Jeshi la Polisi S.L.P 961 DODOMA.
2. Waombaji wote waambatanishe nakala zifuatazo:
  - a) Nakala ya cheti cha kuzaliwa
  - b) Nakala ya kitambulisho cha Taifa cha NIDA au namba ya NIDA
  - c) Nakala ya cheti cha kuhitimu mafunzo ya JKT/JKU kwa walio nje ya makambi.
  - d) Nakala za vyeti vya taaluma (Academic Certificates).
  - e) Nakala za vyeti vya kuhitimu mafunzo ya sekondari (Leaving Certificate).
3. Kwa waombaji wa kidato cha nne ambao wamehitimu mafunzo ya JKT/JKU waliopo nje ya makambi (uraiani) maombi yao yapelekwe kwa Makamanda wa Polisi kwenye Mikoa yao husika na sio Makao Makuu ya Polisi Dodoma.
4. Kwa waombaji wa kidato cha nne waliopo kwenye makambi ya JKT/JKU maombi yao yawasilishwe kwa Makamanda wa Polisi wa Mikoa kupitia kwa Wakuu wa kambi walizopo.
5. Kwa waombaji wenye elimu ya Astashahada na Stashahada zilizoainishwa hapo juu watatakiwa kujaza fomu (kiambatisho 'A') ambayo inapatikana kwenye tovuti ya Polisi inayooonesha taarifa zake binafsi. Utumaji wa fomu hiyo usiwe kwa njia ya kuskani (Scan) ila unatakiwa kupakua (download), na kujaza taarifa husika kisha kuituma pamoja na maombi (Yakiwa kwenye format ya pdf) kupitia barua pepe [admin.phq@tpf.go.tz](mailto:admin.phq@tpf.go.tz). Maombi yote yatakayowasilishwa kwa mkono au kwa njia ya Posta hayatapokelewa.
6. Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 29/07/2023.

Imetolewa na:

**Mkuu wa Jeshi la Polisi Tanzania  
Makao Makuu ya Jeshi la Polisi  
S.L.P 961  
DODOMA  
18/07/2023**